## MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA MWEZI APRILI, 2024 NA MWELEKEO KWA MWEZI MEI, 2024.

### Dondoo za tathmini ya Aprili, 2024 na mwelekeo wa Mei, 2024:

Taarifa hii inatoa muhtasari wa mifumo ya hali ya hewa pamoja na mwenendo wa hali ya hewa kwa mwezi Aprili, 2024 pamoja na mwelekeo wa hali ya hewa kwa mwezi Mei, 2024 nchini.

i. Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2024 vipindi vya mvua vilijitokeza katika baadhi ya maeneo nchini mengi pamoja na vipindi vya mvua kubwa katika baadhi ya maeneo na kusababisha mafuriko, uharibifu wa mali, miundombinu na upotevu wa maisha.
ii. Katika kipindi cha mwezi Mei 2024, mvua zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo hususan yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika maeneo machache.
iii. Joto la kawaida hadi juu kidogo ya kawaida linatarajiwa katika maeneo mengi ya nchi kwa kipindi cha mwezi Mei, 2024.

### 1.0 MUHTASARI WA HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI APRILI, 2024.


Katika kipindi cha mwezi Aprili, 2024 maeneo mengi yaliendelea kupata vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi, pamoja na ongezeko la mvua kwa baadhi ya maeneo. Hata hivyo, uwepo na kuendelea kuimarika kwa Ukandamvua kulisababisha kuongezeka kwa vipindi vya mvua kubwa katika baadhi ya maeneo nchini hususan yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, katika kipindi cha mwezi Aprili 2024, kituo cha Lyamungu kilichopo mkoa wa Kilimanjaro kiliripoti kiwango cha juu zaidi cha mvua cha milimita 179.1 kilichopimwa mnamo tarehe 13 Aprili, 2024 ikifuatiwa na milimita 140 za mvua zilizopimwa katika kituo cha Pemba na milimita 133.5 katika kituo cha Moshi, Kilimanjaro mnamo tarehe 18 na 13 Aprili 2024 mtawalia. Hata hivyo, maeneo ya pwani ya Kaskazini na nyanda za juu Kaskazini Mashariki yalipata vipindi vingi vya mvua kubwa, Vituo vingine vilivyopima mvua milimita 70 au zaidi ni kama inavyoonekana katika kielelezo namba 1.

Kwa upande mwingine, baadhi ya maeneo mengine ya nchi hususan ya ukanda wa pwani yalipata vipindi vya upepo mkali uliofikia au kuzidi kasi ya kilomita 40 kwa saa katika wiki ya tatu na ya nne ya mwezi.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 02/2023*




Kielelezo 1: Vituo vilivyopima viwango vya mvua milimita 70 au zaidi katika mwezi Aprili, 2024

## 2.0 MWELEKEO KWA MWEZI MEI, 2024

### 2.1 MIFUMO YA HALI YA HEWA

Katika kipindi cha mwezi Mei, 2024, joto la Bahari la wastani hadi chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la kati la kitropiki ya Bahari ya Pasifiki, ikiashiria kuendelea kupungua kwa nguvu ya hali ya El Niño. Aidha, joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo kubwa la Bahari ya Hindi. Hata hivyo, eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa na joto la juu zaidi ikilinganishwa na eneo la mashariki. Hali hii inatarajiwa kusababisha upepo wenye unyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea ukanda wa pwani pamoja na mikoa ya jirani. Hali ya joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) inatarajiwa kuwa la juu ya wastani. Hali hii inatarajiwa kusababisha upungufu wa upepo wenye unyevu kutoka misitu ya Congo kuvuma kuelekea maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi.

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa Afrika inatarajiwa kuendelea kuimarika kidogo na hivyo kupelekea Ukandamvua (ITCZ) kusogea kuelekea kaskazini.

## 2.2 HALI YA HEWA KWA KIPINDI CHA MWEZI MEI, 2024

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo za radi vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini. Aidha, ongezeko la mvua linatarajiwa katika baadhi ya maeneo hususani ukanda wa Pwani. Kwa upande mwingine, hali ya joto la kawaida hadi juu kidogo ya kawaida inatarajiwa katika maeneo mengi. Ufuatao ni mwelekeo wa hali ya hewa nchini;

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Pwani, Dar es Salaam, kaskazini mwa mkoa wa Morogoro pamoja na visiwa vya Mafia, Unguja na Pemba):**

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Aidha ongezeko kidogo linatarajiwa hususan kuelekea mwishoni mwa wiki ya kwanza na ya pili ikifuatiwa na upungufu wa mvua katika kipindi kilichosalia cha mwezi.

**Nyanda za juu kaskazini mashariki (Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara):**

Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan wiki mbili za mwanzo za mwezi Mei 2024 ikifuatiwa na upungufu wa mvua katika kipindi kilichosalia. Ongezeko la mvua linatarajiwa katika maeneo machache hususan kati ya wiki ya kwanza na ya pili ya mwezi.

**Kanda ya Ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Mara na Simiyu):**

Vipindi vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo. Upungufu wa mvua unatarajiwa katika maeneo mengi hususan wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Mei, 2024.**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):**

Upungufu wa mvua unatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vichache vya mvua pamoja na ngurumo vinatarajiwa katika maeneo machache hususan katika wiki mbili za mwanzo za mwezi Mei, 2024.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):**

Kwa ujumla, vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo mengi kwa mwezi Mei, 2024.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**Nyanda za juu kusini magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe, Iringa na kusini mwa mkoa wa Morogoro):**

Kwa ujumla, vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo mengi. Aidha, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan yenye miinuko.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):**

Vipindi vya mvua na ngurumo vinatarajiwa katika baadhi ya maeneo. Ongezeko la mvua linatarajiwa hususan katika wiki mbili za mwanzo za mwezi ikifuatiwa na upungufu katika kipindi kilichosalia.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma):**

Kwa ujumla, vipindi vya ukavu vinatarajiwa katika maeneo mengi. Hata hivyo, vipindi vichache vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache hususan yenye miinuko

## 2.3 MATARAJIO KWA MWEZI JUNI, 2024

Katika kipindi cha mwezi Juni, 2024 hali ya joto la chini kidogo kawaida inatarajiwa sambamba na upepo mkali wa Kusi katika baadhi ya maeneo ya nchi.

## 2.4 USHAURI

Mvua zinatarajiwa kuendelea katika baadhi ya maeneo nchini hususani yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka. Aidha, vipindi vifupi vya mvua kubwa vinatarajiwa kujitokeza, hivyo wananchi wanaoishi katika maeneo yanayoathiriwa na mafuriko wanashauriwa kuendelea kuchukua hatua stahiki ili kupunguza athari zitakazojitokeza.

*Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inawashauri watumiaji wa taarifa za hali ya hewa ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, Mamlaka za Wanyamapori, Mamlaka za Maji na Afya waendelee kutafuta, kupata na kufuata ushauri wa wataalamu katika sekta husika.*

Imetolewa tarehe 01 Mei, 2024 na:

**MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA.**

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*
Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610: Nukushi: +255 26 2962610
Barua pepe; met@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz

**(IMETHIBITISHWA – ISO 9001:2015, Huduma za Hali ya Hewa kwa Usafiri wa Anga)**

*727B - 02/2023*